# Karibu katika programu ya Utangulizi!

Swahili



IMDi
Integrerings- og mangfoldsdirektoratet

# Programu ya utangulizi ni kitu gani?

Programu ya utangulizi ni mpango wa mafunzo wenye lengo la kukutayarisha wewe kuweza kushiriki katika maisha ya utendakazi hapa Norway. Wakimbizi wote walio kati ya umri wa miaka 18 – 55 wanapaswa kushiriki katika programu ya utangulizi. Hii inawahusu pia wanafamilia yako watakaoingia hapa nchini wakati ujao.

Kwa kupitia katika programu hii utajifunza lugha na kuweza kuielewa jamii ya Norway. Utapewa mafunzo na elimu ya maisha ya ajira hapa Norway. Ikiwa unataka kuendelea na elimu ya juu utaweza pia kufanya hivyo. Ni moja ya malengo ya kwamba uweze kujiendeleza ki elimu ama uwe mfanyakazi utakapokuwa umemaliza programu.

Programu ya utangulizi inapaswa kuanza haraka sana iwezekanavyo, ikichelewa sana isizidi miezi mitatu baada yaw ewe kuwa mkazi wa manispaa yako.

Programuu ya utangulizi huchukua wakati wote.



## Matarajio yetu kwako

Ni muhimu sana uwe umejitayarisha barabara unapokuja masomoni, na uwajibikie kujifunza unachofundishwa. Mshauri wa programu Pamoja na mwalimu wako watakusaidia. Wanaweza kukushauri na kukuelekeza. Ikitokea kwamba una maswali ni muhimu sana uweze kuzungumza nao.

# Msaada wa kiuchumi

Utakuwa unalipwa kwa wakati wote unapokuwa katika programu ya utangulizi. Msaada huu unaitwa msaada wa utangulizi.

Msaada wa utangulizi unakupatia fursa ya kutofanya kazi nyigine ya mshahara wakati unakuwa masomoni. Ikiwa umri wako ni chini ya miaka 25 na unaishi nyumbani kwa wazazi wako, unapata malipo pungufu kidogo.  Malipo yatokanayo na programu ya utangulizi yanakatwa kodi.  Malipo ya kodi yanakatwa kabla ya  mshahara wako kukufikia.

Ikiwa umepata mapato mengine, pesa za msaada zitapungua. Hii haihusu pesa za Watoto wala pesa za msaada kutoka kwa wazazi waliotengana, au ikiwa unapata pesa kutokana na kazi unazofanya nje ya programu ya utangulizi.

Pesa hizi za programu ya utangulizi hutolewa na manispaa (kommune). Ikigundulika kuwa umetoa maelezo yenye makosa, manispaa yaweza kukudai pesa ulizolipwa kutokana na msaada wa utangulizi.



# Likizo, Kutohudhuria na ruhusa

Una haki ya kuwa na likizo ya majuma matano kwa mwaka. NI haki yako pia ya kuwa na likizo ya ugonjwa, uja uzito na uzazi, au ikiwa kuna sababu nyingine za kimsingi waweza kuruhusiwa usiwe katika programu. Hii tunaita ruhusa. Ni lazima umuombe mshauri wako wa programu ikiwa unataka kupata ruhusa.

Ikiwa kutokuhudhuria kwako hakujakubaliwa na mshauri wako wa programu basi utakatwa malipo yako, na pia muda wako katika programu unapungua.

Ukiamua kuacha masomo katikati ya programu unakosa haki ya kurejea kwenye masomo baadae. Hii husababisha pia kukosa malipo ya programu ya utangulizi.

# Ni nini yaliyomo ndani ya programu ya utangulizi?

Kuna mambo yanayofanana yanayowahusu washiriki wote wa programu, hata hivyo,kuna mambo mengine yanakuhusu wewe tu.

- **Washiriki wote wanapaswa kujifunza lugha ya kinorwey. Mwalimu wako atakupangia lengo lako binafsi. Lengo hili la kujifunza lugha linategemea elimu yako uliyoipata kabla ya kufika hapa.**
- **Washiriki wote wanapaswa pia kujifunza kuhusu jamii na Norwey. Mafunzo haya yatakuwezesha kupata urahisi wa kuishi katika jamii hii ya Norway.**
- **Washiriki wote watafundishwa kozi ya "JInsi ya kuweza kumudu Maisha katika nchi mpya".**
  **Kozi hii itakurahisishia kufanya uchaguzi bora hapa Norway, na kuathiri hali yako mwenyewe. Utweza pia kujua kuwa utapata wapi msaada utakapohitaji.**



Kama unasubiri kujifungua, utapewa miongozo ya kuwa mzazi mwema. Katika miongozo hiyo utaweza kujua jinsi ya kuwa mzazi hapa Norway, na pia kujua fursa kwa ajili yakow ewe mama, na mtoto wako.

Programu ya utangulizi pia itakuwa na sehemu inayokuhusu wewe tu na malengo yako. Hii yaweza kuwa mazoezi ya kufanya kazi bila mshahara, au kwenda kusoma masomo. Wapo wengi ambao hufanya kazi wakati pia wakiwa wanaendelea na masomo yao katika programu ya utangulizi.

Wewe Pamoja na mshauri wako wa programu mtashirikiana kutengeneza mpango kuhusu programu ya utangulizi iwe na masomo ya aina gani yatakavyokufaa wewe.





# Ushauri wa kazi

Kabla ya kuanza programu ya utangulizi utapewa ushauri wa kazi (ajira) Ushauri huu utakuwa unahusu fursa zilizopo kwa ajili yako katika masomo na hatimaye ajira.

Ushauri wa kazi umejengeka kulingana na  maelezo yako kuhusu uzoefu wako na elimu uliyo nayo  kutoka nchini mwako. Yote haya yatakuwa yameshafahamika kabla ya kuanza kupenwa ushauri wa kazi.



# Lengo la mwisho la programu ya utambuisho

Baada ya kupata ushauri wa kazi, wewe pamoja na mshauri wako mtaamua kuwa unapaswa kufikia kiwango gani cha elimu katika programu ya utangulizi. Hii inaweza kuwa lengo la kuendelea na elimu ya juu, au lengo la kupata kazi. Inawezekana pia kuwa ni lengo la kuhitimu masomo yote au sehemu tu ya masomo. Hiyo ndiyo tunaita lengo la mwisho.

Lengo la mwisho kwa ajili ya programu ya utangulizi inatengenezwa kulingana na kile ambacho uliwahi kufanya kule nchini kwako unapotoka iw ni uzoefu wa kazi au ni kiwango cha elimu, na pia mipago yako ya baadae katika maisha yako.

# Programu ya utambulisho ina paswa kuchukua muda gani?

Lengo lako la mwisho ndilo linalotumika kufanya maamuzi ya kwamba utatumia muda gani katika programu ya utangulizi.

Ikiwa ulishasoma shule ya sekondari ya juu katika nchi yako ulikotoka, na lengo lako ni kujiunga na elimu ya juu zaidi au unataka kuanza kazi, basi mud awa programu waweza kuwa miezi sita tu.

Ikiwa lengo lako la mwisho ni kusoma sekondari ya juu, programu ya utangulizi inaweza kufanyika kwa miaka mitatu.

Ikiwa lengo lak la mwisho ni kupata ajira, programu itakuwa ya miaka miwili.

Kuna mazingira yanaweza kusababisha uongezewe muda zaidi katika programu yako.

| LENGO LA MWISHO | MUDA WA PROGRAMU |
|---|---|
| Kukamilisha sekodari ya juu | Miaka mitatu |
| Kazi, au kusoma elimu ya juu | Miezi sita |
| Kazi au kukamilisha sehemu ama kiwango chote cha elimu ya sekondari ya juu | Miaka miwili |

# Tunakutakia kila la kheri katika programu ya utangulizi!



Utgitt av Integrerings- og mangfoldsdirektoratet (IMDi) – 2021.

www.imdi.no